



**KIDATO CHA PILI
MTIHANI WA MWISHO WA
MWAKA 2016
MUDA: MASAA MAWILI**

<i>Tarehe</i>	
<i>Msimamizi</i>	
<i>Kurejeshwa</i>	
<i>Kudurusu</i>	

Maagizo

- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee.

SWALI	UPEO	ALAMA
INSHA	20	
UFAHAMU	20	
SARUFI	40	
ISIMU JAMII	10	
FASIHI SIMULIZI	10	
JUMLA	100	

Jina Nambari ya usajiri..... Dar..... Nambari sahihi

SEHEMU A: INSHA (ALAMA 20)

Andika kadi ya mwaliko ya harusi ya Bi. Perez Ongo na Bw. Ole Tunda wa familia ya Odongo na Masai.

SEHEMU B: UFAHAMU (ALAMA 20)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mwanadamu ni kiumbe aliyeumbwa na Maulana. Katika maisha yake mwanadamu ana mahitaji yake ya kimsingi. Mahitaji haya ni kama chakula, mavazi na **makazi**. Ukosefu wa mambo haya hufanya maisha yake kwenda mbago. Ni tumaini la mwanadamu kuishi maisha mazuri yasiyo na bughudha yoyote.

Licha ya mahitaji ya kimsingi, binadamu anazo haki zinazotambulika na kuidhinishwa kimataifa.

Ni haki ya kila mwanadamu kuishi. Maisha ya binadamu ni kitu bora na chenye kuthaminiwa. Mwanadamu hapaswi, kwa sababu yeyote ile, kutolewa au kujitoa uhai wake.

Ibada ni mojawapo ya matendo yanayomkurubisha mwanadamu na Muumba wake. Hivyo, mtu ana haki mradi tu asimbughudhi mwingine.

Binadamu ana haki ya kujieleza au kutoa maoni bila kudhibitiwa kwa njia yoyote ile. Ni haki ya binadamu **kutangamana** na binadamu wenzake katika **asasi** kama vile vyama vya kishirika, kisiasa, kushughulikia masuala ya kijamii na vinginevyo.

Elimu humwezesha mtu kukabiliana na maisha ipasavyo. Humwezesha pia kujiimarisha kiakili, kiuchumi na kijamii. Ni sharti kila mwanadamu apate elimu.

Kupata huduma bora za afya ni **nguzo** muhimu ya kumstawisha mtu binafsi na jamii kwa jumla. Ni haki ya kila binadamu kupata huduma hizo.

Katika shughuli zake za kila siku, binadamu huweza kujichumia mali. Ana haki ya kuwa nayo na kuitumia mradi tu ameipata kwa njia ya halali.

Mungu aliwaumba binadamu wote wakiwa sawa; weupe kwa weusi, warefu kwa wafupi na wembamba kwa wanene. Mwenyewe ndiye aliywaweka katika hali hizo. Wote wako sawa. Hivyo basi si haki kumbagua binadamu yeyote kwa misingi wa kikabila, dini, rangi, matabaka na kijinsia.

Zilizotajwa hapa ni baadhi tu ya haki za binadamu.

Maswali

1. Taja jambo la kimsingi linalohitajika na mwanadamu. (al.1)

2. Mbali na haki zilizorejelewa, taja haki zingine tatu za kibinadamu. (al.3)

Jina Nambari ya usajiri..... Dar..... Nambari sahihi

-
.....
.....
3. Taja faida mbili za elimu. (al.2)
-
.....
4. Kuna ubaya gani katika kubagua wengine? (al.2)
-
.....
5. Makazi ni muhimu kwa binadamu. Eleza. (al.2)
-
.....
6. Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hiki. (al.4)
- (a) Makazi
- (b) Asasi
- (c) Kutangamana
- (d) Nguzo

SEHEMU C: SARUFI (ALAMA 40)

1. Toa tofauti kati ya silabi huru na silabi funge. (al.2)
-
.....
.....
2. Hizi ni sauti gani? /L/, /r/? Eleza vile zinatamkwa. (al.4)

Jina Nambari ya usajiri..... Dar..... Nambari sahihi

-
.....
.....
.....
.....
3. Toa maana mbili ya neno mboga. (al.2)
-
.....
4. Sahihisha sentensi zifuatazo. (al.4)
- (a) Hii ni mbuzi ambayo itauzwa mnadani.
-
.....
- (b) Hapa ndimo alikookota saa hii.
-
.....
5. Bainisha viambishi katika sentensi hii. (al.6)
- Alinisahaulia
-
.....
.....
.....
6. Weka nomino zifuatazo katika ngeli zao. (al.4)
- (a) Okello
- (b) Manukato
- (c) Tarumbeta
- (d) Kengele
-
.....
7. Tumia kivumishi –ote na maneno yafuatayo katika sentensi. (al.4)

Jina Nambari ya usajiri..... Dar..... Nambari sahihi

(a) Msichana

.....

(b) Chakula

.....

8. Tambua na uainishe vitenzi vifuatavyo. (al.4)

(a) Cheza

(b) Kuwa

(c) Ngali

9. Eleza tofauti kati ya: (al.2)

(a) Shadda

(b) Kiimbo

10. Andika maneno yenye miundo hii. (al.3)

(i) KKI

(ii) KKKI

(iii) KKKKI

11. Onyesha maana mbili za sentensi hii. (al.2)

Mama alimsomea mtoto wake

.....

.....

12. Pambanua aina za maneno katika sentensi hii. (al.3)

Tunda li mtini

.....

.....

SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Jina Nambari ya usajiri..... Dar..... Nambari sahihi

Taja na ueleze sifa tano zozote za lugha ya sokoni.

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)

- (a) Eleza maana ya utanzu wa maigizo. (al.2)

- (b) Eleza hoja nne zozote za dhima ya maigizo. (al.8)